**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KWENYE KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA WAFANYAKAZI DUNIANI (MEI MOSI)

**ARUSHA**

**1 MEI, 2024**

***Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***

***Mhe. Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati;***

***Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;***

***Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania;***

***Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM);***

***Mhe. Jenista Joachim Mhagama (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu;***

***Mhe. Deogratias John Ndejembi (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu- Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu;***

***Wahe. Mawaziri na Naibu Mawaziri mliopo;***

***Mhe. Dkt. Moses Mpogole Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi;***

***Mhe. Paul Christian Makonda, Mkuu wa Mkoa wa Arusha;***

***Komredi Thomas Ole Sabaya, Mwenyekiti wa CCM - Mkoa wa Arusha;***

***Ndg. Tumaini Nyamhokya, Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA);***

***Mhe. Caroline Mugala, Mkurugenzi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), Ofisi ya Kanda ya Afrika Mashariki;***

***Wahe. Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Kimataifa mliopo;***

***Wahe. Wabunge mliopo;***

***Mhe. Dkt. Yose Mlyambina, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu - Divisheni ya Kazi;***

***Ndg. Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu mliopo;***

***Ndg. Herry Mkunda, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA);***

***Ndg. Oscar Mgaya, Mwenyekiti wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE);***

***Bi. Suzan Ndomba Doran, Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE);***

***Bi. Suzan William Mkangwa, Kamishna wa Kazi;***

***Bw. Donald Allacka, Kaimu Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri;***

***Viongozi Wakuu wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) mliopo;***

***Wahe. Wakuu wa Mikoa na Wilaya mliopo;***

***Viongozi wa Taasisi za Umma na Sekta Binafsi mliopo;***

***Dkt. Samuel Nyantahe, Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri wa Masuala ya Kazi, Kiuchumi na Jamii (LESCO);***

***Dkt. Suleiman Mohamed, Mwenyekiti wa Bodi ya Kima Chini cha Mshahara Sekta Binafsi;***

***Dkt. Lucas Kija, Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Watu Wenye Ulemavu;***

***Wahe. Viongozi wa Dini mliopo;***

***Viongozi Waandamizi wa Serikali mliopo;***

***Wawakilishi wa Vyama vya Siasa mliopo;***

***Wafanyakazi wenzangu pamoja na Wananchi mliokusanyika hapa; Wanahabari; Mabibi na Mabwana.***

***Mshikamano, .........Solidarity.......!***

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.....!***

Nimepewa heshima kubwa sana ya kumwakilisha Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika sherehe hii muhimu sana ya Mei Mosi mwaka huu 2024. Napenda nami nianze kwa kuongeza sauti yangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia neema ya uhai na kutuwezesha kukutana hapa kwa ajili ya kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani.

Ninawashukuru sana viongozi wa TUCTA kwa kumualika Mhe. Rais pamoja na viongozi wengine wakuu wa kitaifa ili kuungana na wafanyakazi wote nchini kuadhimisha siku hii kubwa kote duniani. ***Ahsanteni sana!*** Aidha, ninawapongeza kwa maandalizi mazuri na kwa maadhimisho yaliyofana. ***Hongereni sana.*** Nimefurahi kuona kwamba, sherehe za mwaka huu, zimeratibiwa na vyama 13 vya wafanyakazi, vikiwemo vile ambavyo siyo wanachama wa TUCTA. Hakika hii ni hatua nzuri katika kuimarisha mshikamano baina ya wafanyakazi wote. Ninawashukuru pia kwa namna tunavyoendelea kushirikiana kupitia ubia wetu baina ya Serikali, waajiri na vyama vya wafanyakazi.

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi;***

Kati ya mwaka jana na sasa, wapo wafanyakazi wenzetu ambao wamepatwa na changamoto mbalimbali za kiafya na wengine wamepoteza maisha. Naomba nitumie fursa hii, kuwapa pole wale wote wenye changamoto za kiafya, na kwa wale waliotangulia mbele za haki, tumuombe Mungu azipumzishe roho zao mahala pema peponi. Amina.

Naomba pia nitumie hadhira hii kuwapongeza wafanyakazi wote nchini, na kuwashukuru kwa juhudi kubwa wanazofanya katika maeneo yao ya kazi, ambazo kwa hakika zimesaidia kuendelea kusukuma mbele maendeleo ya Taifa letu. ***Ahsanteni sana!*** Kwa wale wafanyakazi wachache wasiotimiza wajibu wao ipasavyo, ninawaasa watumie siku hii kujitafakari na waamue kwa dhati kubadilika! Aidha, napenda nitumie fursa hii kuwaomba wenzetu katika vyama vya wafanyakazi, tusaidiane katika kusisitiza maboresho ya kiutendaji miongoni mwa wanachama wenu, sambamba na kutumia maadhimisho ya Mei Mosi kupendekeza maboresho mbalimbali ya maslahi ya wafanyakazi kama ilivyo ada. Hatua hii itasaidia kuongeza uelewa kwamba, ***haki inaendana na wajibu!***

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi;***

Serikali imesikiliza kwa makini risala yenu, ambayo imetoa mrejesho mzuri kuhusu jitihada mbalimbali za kuleta ustawi wa wafanyakazi na Watanzania wote kwa ujumla. Ninawashukuru sana kwa kutambua kwamba, yapo mengi yanayofanyika, ambayo yanalenga katika kuimarisha ustawi wa wafanyakazi. Kwenye risala hiyo mmetoa ushauri kwa Serikali na kuibua hoja mbalimbali. Hivyo basi, naomba mniruhusu nitoe ufafanuzi kuhusu ushauri na hoja hizo kama ifuatavyo:

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi;***

**Kuhusu Bodi za Kima cha Chini cha Mshahara** kuundwa na kuanza kazi zake mapema. Napenda niseme tu kwamba Serikali inashukuru kwa ushauri huo. Kwa upande wa Bodi ya Kima cha Chini cha Mishahara katika utumishi wa umma, Bodi hiyo iliundwa mwaka 2016 na kumaliza muda wake mwaka 2023, na tayari Bodi mpya imeundwa na inaendelea na majukumu yake. Aidha, ninapenda kuwafahamisha kwamba, Bodi hiyo kwa upande wa Sekta Binafsi iliundwa Aprili, 2022 na bado ipo hai. Bodi hii ilikuwa na mchango mkubwa katika kufikia uamuzi wa kima kipya cha chini cha mshahara kwa Sekta Binafsi kilichotangazwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 687 tarehe 25 Novemba, 2022 na kuanza kutumika tangu Januari, 2023.

Kama mnavyojua, Sheria inataka Bodi hiyo kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha miaka mitatu (3) na Amri ya Kima cha Chini cha Mshahara hufanyiwa mapitio ndani ya kipindi hicho. Kwa kuzingatia matakwa hayo ya Kisheria, tayari tumeanza utafiti wa kina wa Kima cha chini cha Mshahara kwa Sekta Binafsi

ambao utajumuisha sekta ndogo ndogo kwa upana zaidi. Natoa wito kwa wajumbe wa Bodi kutoka TUCTA kushiriki kikamilifu katika mchakato huo ili tufikie uamuzi shirikishi utakaosadifu mazingira ya wakati uliopo.

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi;***
Risala yenu pia imewasilisha hoja kuhusu **kufuta vifungu kwenye mikataba ya halibora bila kuzingatia makubaliano ya pande mbili**. Ndugu zangu, Serikali inatambua fika umuhimu wa motisha kwa watumishi katika kuongeza tija. Ndiyo maana tumekuwa tukiidhinisha mipango ya motisha au kuridhia mikataba ya halibora ya Taasisi za Umma kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura 366. Hapa ni vema tukumbushane kuwa, pamoja na Mikataba ya Halibora kutamkwa katika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 imempa mamlaka Katibu Mkuu UTUMISHI kuidhinisha mikataba hiyo.

Sheria hiyo ililenga kuleta uendelevu katika utekelezaji wa mikataba hiyo kwa kuzingatia uwezo wa kibajeti. Sheria hiyo pia imebainisha kuwa endapo kuna ukinzani katika masuala ya kiutumishi na maslahi, kati ya Sheria ya Utumishi na Sheria nyingine, basi Sheria ya Utumishi wa Umma itatumika. Kwa muktadha huo, maboresho yanayofanywa na Katibu Mkuu UTUMISHI kwenye mikataba ya halibora, hayavunji sheria. Pamoja na maelezo hayo ya kisheria, Serikali ina maoni kwamba, Mkataba wa halibora wenye maslahi machache yanayotekelezeka, ni muhimu zaidi ya ule wenye maslahi mengi lakini usiotekelezeka.

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi;***
Kuhusu hoja ya **watumishi walioko kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kulipwa mishahara kupitia Mfuko mkuu wa Serikali**; tunakubaliana na hoja hii na Serikali inaendelea na utekelezaji wake kwa awamu. Kuanzia mwezi Julai, 2024 watumishi 473 kutoka Halmashauri 101 zilizobainika kutokuwa na uwezo wa kulipa mishahara ya watumishi wake kwa kutumia mapato ya ndani, sasa tutawalipa kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali. Kiasi cha Shilingi 3,530,244,000.00 zimetengwa kwa ajili hiyo. Aidha, Serikali itaendelea kufanya tathmini ya mara kwa mara ili kubaini uwezo wa kifedha wa Halmashauri husika na kufanya uamuzi kadri itakavyoonekana inafaa. Pamoja na kusema hayo, ni matarajio ya Serikali kwamba, Halmashauri husika zitasimamia vizuri fedha za vyanzo vya mapato ya ndani, na kuboresha huduma za kijamii. Aidha, ni lazima Halmashauri ziendelee kuongeza ubunifu ili kupata vyanzo vipya vya mapato na kusimamia kikamilifu matumizi yake.

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi;***
Serikali imeisikia hoja ya **kuirejesha SSRA**, ikiwa ni miaka mitano baada ya kufanya uamuzi wa kuifuta na kuunda Idara chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi,

Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kusimamia Sekta hiyo. Idara hiyo ilirithi majukumu yote ya usimamizi na udhibiti yaliyokuwa chini ya SSRA na Benki Kuu ya Tanzania kusimamia masuala yote yanayohusu uwekezaji. Ushauri wenu wa kufikiria upya uamuzi huo wa mwaka 2019 tumeupokea na tutaendelea kuutathmini kisha uamuzi utafanyika kwa kuzingatia ushauri wa kitaalamu na uhalisia wa kiuendeshaji kwenye sekta ya hifadhi ya jamii.

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi;***

**Kuhusu ajira za mikataba,** Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura 366 imeainisha aina mbalimbali za mikataba ikiwemo Mkataba wa muda maalum kwa wataalam na mameneja, mkataba usio wa muda maalum (wa kudumu) na mkataba wa kazi maalum. Kwa mujibu wa Sheria tajwa, wafanyakazi wanaoajiriwa kupitia mikataba ya aina zote, wanastahili kupata haki mbalimbali ikiwepo Bima ya Afya, kuunganishwa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na mikopo kwa kuzingatia vigezo na masharti ya Taasisi husika.

Aidha, Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za mwaka 2009, zimeainisha aina mbalimbali za ajira ikiwa ni pamoja na Ajira ya masharti ya kudumu na mafao ya uzeeni, Ajira ya muda maalum (mkataba) na Ajira ya kazi maalum. Kupitia mikataba tajwa, haki na stahiki mbalimbali za watumishi zimeainishwa. Mfano; watumishi wanaoajiriwa kwa mkataba wanayo haki ya kulipwa kiinua mgongo baada ya kuhitimisha mikataba yao. Aidha, watumishi wanaoajiriwa kwa kazi maalum wanalipwa stahili zao kulingana na kazi walioajiriwa kutekeleza. Ndugu wafanyakazi, ni wazi kwamba kazi za mikataba haziepukiki katika ulimwengu wa kazi. Hivyo, jambo la muhimu hapa ni kuendelea kuhakikisha ajira hizo zinazingatia misingi ya kazi za staha.

Kuhusu **wakala wa ajira kujibadili kuwa kama waajiri**, Serikali inakubaliana na hoja kwamba jambo hili ni kinyume cha sheria na halikubaliki. Jukumu la msingi la Mawakala kwa mujibu wa Sheria ya Kukuza Huduma za Ajira, linabaki kuwa ni kuunganisha watafuta kazi na waajiri . Kwa mujibu wa Sheria hiyo, ni kosa kwa wakala kugeuka kuwa waajiri wa watafuta kazi. Hivyo, Serikali imepokea ushauri wenu kuhusu umuhimu wa kuendelea kuwasimamia Mawakala ili watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa sheria. Katika kuimarisha usimamizi wa Mawakala, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kudhibiti vitendo vya Mawakala kugeuka kuwa waajiri. Hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu kwa Mawakala kuhusu majukumu yao kwa mujibu wa sheria, kufanya ukaguzi na kuwafanyia upekuzi endelevu kabla ya kuwapa leseni kwa lengo la kujiridhisha na mienendo yao ya kiutendaji na uzingatiaji wa sheria. Sambamba na hatua hizo, Serikali itaendelea na hatua za kuifanyia marekebisho Sheria ya Kukuza Huduma za Ajira kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa Mawakala hao.

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi;***

Kuhusu **changamoto za ajira rasmi na upungufu wa ujuzi na stadi muhimu za kuweza kujiajiri**. Mmetushauri kutumia fedha za SDL katika kuongeza ujuzi. Tunawashukuru sana kwa ushauri wenu, ambao unaendana na mwelekeo wetu kama Serikali kutilia mkazo uboreshaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Katika hili, tayari tumeboresha Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 ambapo Toleo la mwaka 2023 limeanza kutumika tangu mwezi Januari 2024. Ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba Sera hii inaleta matokeo yaliyokusudiwa.

Serikali pia inatambua umuhimu wa **kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi** nchini ili kuwezesha vijana kupata mafunzo na stadi zitakazo wawezesha kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Katika hili, Serikali imechukua hatua zifuatazo;

(i) Imekamilisha ujenzi wa Vyuo vya VETA 29 ambapo 25 ni vya Wilaya na 4 ni vya ngazi ya Mkoa;
(ii) Inakamilisha ujenzi wa Chuo Cha Ufundi Dodoma na ujenzi umefikia takriban asilimia 97;
(iii) Inaendelea na ujenzi wa vyuo vya VETA 65 (64 vya Wilaya na Kimoja cha Mkoa wa Songwe);
(iv) Inaendelea na ujenzi wa Kampasi 14 za Vyuo Vikuu zenye kujielekeza kutoa elimu ya mafunzo kwa vitendo; na
(v) Imeanza ujenzi wa shule za Ufundi 100 katika Halmashauri zisizo na Taasisi za Elimu ya Ufundi.

Hatua hizi zimewezeshwa na fedha za Serikali na mchango wa Sekta Binafsi ikiwemo fedha za Uendelezaji Ujuzi (SDL). Vilevile, Serikali kwa kutumia fedha za SDL inatekeleza Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi ambayo inatoa mafunzo ya Uanagenzi, Mafunzo ya Utarajali (mafunzo ya uzoefu wa kazi katika maeneo ya kazi), Mafunzo ya Kurasimisha Ujuzi uliopatikana nje ya Mfumo Rasmi wa Elimu (RPL), Mafunzo ya kuongeza Ujuzi kwa Walio Kazini (*re-skilling/upskilling*), Mafunzo ya Kilimo kwa Teknolojia ya Kitalu Nyumba, Unenepeshaji Wanyama na Mafunzo ya Ufugaji Viumbe Maji. Kupitia programu hizi, jumla ya vijana **141,968** wamenufaika na vikundi vya vijana **219** vyenye jumla ya vijana **1,317** walionufaika na programu wamewezeshwa vifaa na vitendea kazi (*tool kits*) kwa ajili ya kufanyia kazi na kuendeleza ujuzi walioupata kwa kujiajiri ama kuajiriwa.

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi***

Serikali imepokea ushauri wa TUCTA kuhusu **kuridhia Mikataba yote muhimu inayogusa masuala ya wafanyakazi** nchini na kukamilisha uridhiaji wa Mikataba 6 ya ILO iliyoanza kushughulikiwa. Serikali inatambua umuhimu wa kuridhia Mikataba ya ILO inayogusa maslahi ya wafanyakazi.

Mpaka sasa, baada ya kupitia na kujiridhisha kuhusu yaliyomo ndani, Serikali imeridhia Mikataba minane (8) kati ya 10 ya Msingi (*Core Conventions)*. Aidha, Serikali imeshaanza mchakato wa kuridhia Mikataba Sita (6) ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) ambayo inajumuisha Mikataba miwili (2) ya Msingi iliyobaki.

Serikali inapenda kusisitiza kwamba, kuridhiwa kwa mikataba ya kimataifa kutafanyika baada ya kujiridhisha na masuala ya msingi kama vile mila, tamaduni, desturi na maslahi mapana ya nchi yetu kwa ujumla. Kwa sasa tunaendelea na michakato ya ndani ya Serikali, na baada ya hatua hiyo, mapendekezo yatawasilishwa Bungeni kwa hatua zaidi.

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi;***

**Kuhusu mifumo ya utatuzi wa migogoro ya kikazi,** Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 Marejeo ya Mwaka 2019, imeainisha utaratibu wa kufuata katika kushughulikia migogoro ya kikazi katika Utumishi wa Umma. Aidha, Sheria inawataka watumishi wa Umma kutumia njia zote za kurekebisha (remedies) zilizoainishwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma kwa kutumia Sheria nyingine ikiwemo Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura 366.

Aidha, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuimarisha utendaji wa Tume ya Utumishi wa Umma ikiwemo kuongeza idadi ya siku za mikutano ya Tume kutoka siku 10 hadi 15 ili kushughulikia rufaa na malalamiko mengi zaidi, kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye Wizara na Taasisi za Umma kwa lengo la kuangalia uzingatiwaji wa Sheria katika usimamizi wa rasilimaliwatu na hivyo kupunguza rufaa na malalamiko ya watumishi, kuwajengea uwezo watumishi wa Tume na kuweka Mfumo wa Kielektroiniki wa kushughulikia rufaa na malalamiko.

Serikali imepokea pia ushauri kuhusu **kuiongezea Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) watumishi na vitendea kazi** ili kuiwezesha kufanya kazi kwa ufanisi. Aidha, kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali itaendelea kuboresha utoaji wa huduma za CMA kwa kuipatia vitendea kazi ikiwemo magari na kuongeza idadi ya watumishi kulingana na uwezo wa kibajeti. Mfano, kwa mwaka wa fedha wa 2021/22 Serikali ilitoa kibali kwa Tume cha kuajiri watumishi 8, mwaka 2022/23 watumishi 16 na 2024/25 nafasi 24 zimetengwa kwa ajili ya ajira mpya. Aidha, Serikali inaendelea kusimika Mifumo ya Kielektroniki ya usajili, utatuzi na usimamizi wa migogoro ya kazi. Mifumo hii itawezesha Wafanyakazi na Waajiri popote walipo kusajili migogoro ya kazi ikiwemo kutumia simu-janja pasipo kulazimika kuzifuata Ofisi za CMA. Utaratibu huu ni kama inavyofanyika katika Mahakama kote nchini.

Kuhusu **utaratibu wa kupata Vibali vya Ajira** katika Utumishi wa Umma kwa makundi mbalimbali, huu ni utaratibu wa kawaida uliowekwa kwa mujibu wa Sheria. Napenda nitumie fursa hii kusisitiza kwamba, watumishi wa taasisi

za serikali ambazo zimeundwa kwa sheria mbalimbali wote ni watumishi wa umma. Hivyo, ni lazima kufuata sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza ajira katika utumishi wa umma. Utaratibu huu unalenga kuimarisha udhibiti katika eneo la ajira ambalo linapaswa kuzingatia sifa, uwezo wa kibajeti na vipaumbele vya Serikali katika kulitekeleza. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba eneo hili linaendelea kuwa na ufanisi ili kuharakisha utoaji wa Vibali vya Ajira kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo.

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi;***

**Kuhusu Bima ya Afya**, katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora za matibabu nchini, Serikali imefanya maboresho katika Orodha ya Taifa ya Dawa Muhimu (NEMLIT) pamoja na Miongozo mbalimbali ya Tiba (STG). Hivyo, kutokana na maboresho hayo, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umefanya maboresho katika Kitita chake ili kwenda sambamba na Miongozo hiyo kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma bora kwa wanachama wake. Hata hivyo, kutokana na changamoto zilizojitokeza baada ya kuanza utekelezaji wa Kitita hicho, Serikali iliunda Kamati huru ya Wataalam ili kupitia hoja za wadau na kupata suluhu ya changamoto zilizojitokeza. Kwa kuwa zoezi la mapitio ya Kitita bado linaendelea, Serikali itahakikisha wadau wote muhimu wanashirikishwa kikamilifu katika zoezi hilo na kutatua changamoto zilizojitokeza. Aidha, nimetaarifiwa kuwa tayari TUCTA wamekutana na NHIF tarehe 25/4/2024 na kutoa ufafanuzi wa hatua zilizochukuliwa kutokana na changamoto zilizojitokeza.

Uhai na uendelevu wa Mifuko ya Bima ya Afya Duniani kote unategemea uwasilishaji wa michango ya Wafanyakazi kwa wakati kutoka kwa Waajiri. Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Sura 395, inataka kila Mwajiri kuwasilisha mchango wa bima ya afya ndani ya siku 30 tangu tarehe ya malipo ya mshahara wa Mfanyakazi. Kwa kutambua jukumu hilo, Serikali imekuwa ikiwasilisha michango ya Watumishi wa Umma kwa wakati. Ili kuepusha usumbufu kwa Wafanyakazi, Waajiri wote wanaojiunga kwa hiari katika Mfuko wanakumbushwa kuwasilisha kwa wakati michango ya Wafanyakazi wao.

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi;***

**Kuhusu likizo ya uzazi kwa wafanyakazi wanawake wanaojifungua mtoto/watoto njiti.** Suala la afya ya mama na mtoto ni suala ambalo Serikali inalipatia kipaumbele kikubwa sana. Katika miaka hii mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita, tumeshuhudia uwekezaji mkubwa katika kuboresha huduma za afya ya mama na mtoto kote nchini, ikiwemo usambazaji wa vifaa vya huduma kwa watoto wachanga na wenye uzito pungufu.

Taarifa ya Utafiti wa Afya ya Mama na Mtoto na Viashiria vya Malaria nchini *(Tanzania Health and Demography Survey)* uliofanyika mwaka 2022, unaonesha vifo vitokanavyo na uzazi kupungua kutoka vifo **530 kwa kila vizazi hai**

**100,000** mwaka **2015-16** hadi kufikia vifo **104** kwa kila vizazi hai **100,000** mwaka 2022, Taarifa pia inaonesha kuendelea kupungua vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano kutoka **67** kwa kila vizazi hai **1,000** mwaka 2015/16 hadi kufikia vifo **43** kwa kila vizazi hai **1,000**. Uwekezaji kwenye sekta ya afya umelenga kuhakikisha kwamba watoto na wanawake kwa ujumla wakiwemo watumishi wanapata huduma bora.

Napenda kusisitiza kwamba likizo ya uzazi ni miongoni mwa haki za mfanyakazi na hutolewa kwa muda wa siku 84 endapo mfanyakazi atajifungua mtoto mmoja au siku 100 endapo mfanyakazi atajifungua mtoto zaidi ya mmoja. Iwapo mfanyakazi atajifungua mtoto au watoto kabla ya muda wake, mtoto au watoto husika huwekwa katika chumba na mashine maalum (*incubator*) chini ya uangalizi wa madaktari na wahudumu wengine wa afya hadi pale wataalam hao wanapojiridhisha kuwa afya ya mtoto/watoto hao imeimarika. Hivyo, iwapo mfanyakazi atajifungua mtoto au watoto njiti, kipindi cha uangalizi maalumu hakitahesabiwa kama likizo ya uzazi. Likizo ya uzazi itaanza pale mtoto atakapomaliza kipindi cha uangalizi maalum kadri madaktari watakavyothibitisha. Vilevile, mfanyakazi husika ataruhusiwa kutoka kazini saa 7:30 kila siku kwa muda wa miezi sita baada ya kumalizika kwa likizo ya uzazi ili kumpa fursa ya kwenda kunyonyesha.

Kwa upande wa likizo ya uzazi kwa wafanyakazi wa Sekta Binafsi, Serikali inatambua umuhimu wa kulinda haki ya mama na mtoto hususan watoto njiti. Aidha, Serikali ipo katika hatua ya kuifanyia marekebisho Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini, Sura 366 ili likizo ya uzazi ianze pale mtoto atakapomaliza kipindi cha uangalizi maalum kadri madaktari watakavyothibitisha.

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi;***

Kuhusu hoja ya **kuboresha Kanuni ya ukokotoaji wa mafao**, Serikali imepokea ushauri uliotolewa. Hata hivyo, ni muhimu kuzingatia kwamba uendeshaji na usimamizi wa mifuko ya hifadhi ya jamii ni suala la sayansi ya Watakwimu-bima (*actuarial science).* Hivyo, tunawategemea wataalam wetu watushauri kuhusu suala hili la uhimilivu na uendelevu wa mifuko ya hifadhi ya jamii. Mhe. Rais na Serikali yake tunawahakikishia wafanyakazi kwamba hakuna mtu ambaye angependa kuona watu walioitumikia nchi hii, wakiathirika kwa kukosa kiinua mgongo stahiki au pensheni zao. Kutokana na hali hiyo, ndiyo maana Serikali iliposhauriwa na wataalam husika, Serikali ya Awamu ya Sita ilichukua uamuzi mkubwa wa kulipa deni la mifuko ya Hifadhi ya Jamii kiasi cha **shilingi trilioni 2.147,** hatua ambayo kwa kiasi kikubwa imeimarisha mifuko hiyo. Vilevile, tumeendelea kuimarisha utendaji kwenye mifuko hiyo na kupunguza ucheleweshaji wa malipo ya wastaafu.

Kwa hiyo, kwa kifupi Serikali imepokea hoja kuhusu kubadilisha kikokotoo kwa ajili ya kuifanyia uchambuzi zaidi, maana kama ilivyosemwa kwenye risala,

wafanyakazi hawaridhishwi na kanuni hizo. Hata hivyo, uamuzi wa kubadilisha Kikokotoo ni lazima utokane na tathmini ya kina ya kisayansi ya Watakwimu-bima. Ni matumaini ya Serikali kwamba, TUCTA itashiriki kikamilifu katika zoezi hilo na kuwasilisha maoni yatakayoimarisha zaidi mifuko.

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi;***

Kuhusu hoja ya **kodi kwenye mapato yasiyo ya mshahara**, naomba nieleze kwamba, kodi katika mapato ya wafanyakazi inatozwa kwa mujibu wa Sheria na utaratibu wa ukokotoaji, na ukusanyaji unazingatia kanuni za msingi za utozaji kodi ikiwemo kuweka usawa kwa watu wenye kipato kinachofanana.

Utaratibu huo pia unawezesha udhibiti wa vitendo vya baadhi ya waajiri wasio waaminifu, kufanya udanganyifu kwa kupunguza kiasi cha msingi cha mishahara na kuainisha kwenye mahesabu yao kiasi kikubwa cha posho na marupurupu ili kukwepa wajibu wa kulipa kodi na michango ya pensheni za wafanyakazi wao, ambazo ni haki ya msingi kwa ajili ya kuwawezesha kupata kipato cha kujikimu baada ya kustaafu. Kama sehemu ya kaulimbiu ya mwaka huu isemavyo, ***"Nyongeza ya Mishahara ni Msingi wa Mafao Bora....".*** Kwa wale waajiri wanaoficha mishahara katika posho, watambue kuwa licha ya kuikosesha Serikali mapato, pia wanawakosesha wafanyakazi wao mafao bora baada ya kustaafu. Kwa muktadha huo, Serikali itaendelea kusimamia Sheria ya Kodi ili kulinda haki za wafanyakazi.

Napenda nitumie fursa hii kutambua mchango mkubwa wa wafanyakazi katika ulipaji wa kodi. Kimsingi, wafanyakazi ni miongoni mwa walipaji wazuri wa kodi, na mnayo kila sababu ya kujipongeza kwa mchango wenu adhimu kwa Taifa. Kupitia sherehe hizi za Mei Mosi, naomba niendelee kuyasihi makundi mengine katika jamii, kutimiza wajibu wao wa kisheria wa kulipa kodi kwa maendeleo ya Taifa. Napenda nitumie fursa hii pia kuwasihi wafanyakazi wote nchini, kuwa mstari wa mbele katika kudai risiti kila wanaponunua bidhaa au huduma, na wahakikishe risiti wanazopewa zimeandikwa gharama halisi. Kwa kufanya hivyo, siyo tu tutaiwezesha Serikali kupata mapato zaidi ya kuimarisha ustawi wa jamii ambayo wafanyakazi ni sehemu yake, bali pia itaipa Serikali wigo mpana zaidi wa kuboresha maslahi ya wafanyakazi.

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi;***

Serikali inakubaliana na Kaulimbiu ya mwaka huu isemayo, "**Nyongeza ya Mishahara ni Msingi wa Mafao Bora na Kinga Dhidi ya Ugumu wa Maisha".** Kwa tafsiri, kaulimbiu hii inamzungumzia mfanyakazi aliye kazini na yule aliyestaafu. Lakini zaidi, inahusu pia wananchi wengine kwa ujumla. Kwa niaba ya Serikali napenda kuwahakikishia kuwa tunatambua umuhimu wa kupunguza ugumu wa maisha ya wananchi wote ikiwemo watumishi. Ni kwa

sababu hiyo, tumekuwa tukichukua hatua mbalimbali za kuwahami wananchi dhidi ya ugumu wa maisha, kama mlivyobainisha wenyewe kwenye risala yenu.

Mathalan, kufuatia ongezeko la bei ya mafuta kwenye soko la dunia baada ya kuanza kwa vita baina ya Urusi na Ukraine, Serikali ilichukua hatua za haraka na za muda maalum za kuweka ruzuku ya mafuta, ili kuwakinga wananchi wote dhidi ya athari ambazo zingesababishwa na ongezeko kubwa na la ghafla la bei ya mafuta. Vilevile, Serikali imeendelea kudhibiti mfumuko wa bei, katika kiwango cha wastani wa **3.9%,** kwa kusimamia utekelezaji wa sera za fedha na matumizi ya Serikali. Aidha, tumeendelea kuhakikisha nchi inakuwa na utoshelevu wa chakula ambapo Serikali imeendelea kutoa ruzuku ya mbolea na pembejeo za kilimo. Kwa sasa utoshelevu wetu wa chakula ni zaidi ya **100%.** Hii ina maana kwamba tuna chakula zaidi ya mahitaji yetu wenyewe nchini. Ndugu zangu, hatua zote hizi, zililenga kuleta ahueni kwa wananchi, wakiwemo wafanyakazi. Hatua nyingine tulizochukua kuleta ahueni zaidi kwa wananchi na wafanyakazi kwa ujumla ni kama mlivyosema kwenye risala yenu kuhusu uwekezaji mkubwa tuliofanya kwenye sekta mbalimbali za huduma za jamii hususan elimu, afya, maji, nishati ya umeme na miundombinu ya usafirishaji na mawasiliano.

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi;***

**Kuhusu nyongeza ya mishahara,** kama mlivyosema kwenye risala yenu, mwaka wa Fedha 2022/23 Serikali ilipandisha kima cha chini cha mshahara kwa asilimia 23.3 kutoka shilingi 300,000 hadi shilingi 370,000 kwa mwezi. Lengo la kutoa nyongeza kwa kiwango hicho lilikuwa ni kuwezesha watumishi wenye mishahara ya kima cha chini kumudu gharama za maisha kwa kadri inavyowezekana. Makundi mengine ya watumishi nayo yaliguswa na ongezeko hilo la mshahara kwa viwango tofauti kwa kuzingatia ukomo wa bajeti ya mshahara iliyotengwa. Kama ambavyo tumekuwa tukisema, Serikali itaendelea kuhuisha viwango vya mshahara kwa kuzingatia uwezo wa kiuchumi na kibajeti pamoja na ujuzi na utendaji wa waajiriwa. Misingi hii ni muhimu ili kuepuka kuchochea mfumuko wa bei, kuhatarisha uhimilivu wa deni la Taifa na athari nyingine kwenye utulivu wa uchumi wa Taifa kwa ujumla. Haya yote lazima yazingatiwe katika mchakato wa kuongeza mishahara, hususan katika kipindi hiki ambapo uchumi wa dunia umekumbwa na misukosuko mingi ikiwemo vita baina ya Urusi na Ukraine, vita ya Mashariki ya Kati inayohusisha Israel, Palestina, Lebanon, Syria, Iran na Yemen. Vita hivyo vimepelekea kuvurugika kwa mfumo wa ugavi na kupanda sana kwa bei za mafuta, mbolea, chuma na chakula. Kama hiyo haitoshi, dunia imekumbwa na majanga mengine ikiwemo mvua kubwa na maporomoko ya ardhi ambayo yamesababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu, magonjwa na hata vifo. Changamoto zote hizi zimeathiri uchumi wetu. Pamoja na changamoto hizi, tathmini ya Serikali na ya

Taasisi za kimataifa ikiwemo IMF, Benki ya Dunia, AfDB, Moody's, Fitch n.k. zimeonesha kuwa uchumi wa Taifa umekuwa stahimilivu kwa kiasi cha kuridhisha *(resilient to global shocks)*, nchi yetu inakopesheka na ina mvuto kwa wawekezaji wa moja kwa moja kutoka nje. Hivyo, Mama ameniagiza niwaambie wafanyakazi wa Tanzania kuwa endapo hali hii itadumu, wawe na matumaini kwamba atasema jambo hivi karibuni.

Pamoja na hatua hiyo, Serikali imeendelea kuboresha maslahi ya watumishi kwa namna nyingine mbalimbali, ikiwemo kwa kulipa nyongeza ya mwaka ya mshahara *(annual salary increment)*, ambapo Mwaka 2023/24 kiasi cha shilingi 153,926,496,703.68 kililipwa; na kwa mwaka 2024/25, Serikali imetenga shilingi 150,873,245,100.00 kwa ajili hiyo. Kama mlivyosema kwenye risala yenu, kabla ya mwaka jana, nyongeza ya mshahara ilikuwa imesimama kwa muda mrefu, lakini sasa tunajitahidi kuitekeleza. Kwa upande mwingine, Serikali imeendelea kuwapandisha vyeo watumishi mbalimbali, ambapo Mwaka 2023/24 jumla ya watumishi 81,515 walipandishwa vyeo na mwaka 2024/25 Serikali imetenga kiasi cha 252,703,717,483.72 kwa ajili ya kuwapandisha vyeo watumishi 219,924.

***Ndugu Viongozi na Wafanyakazi:***

Kwa kuhitimisha, napenda kuwapongeza tena wafanyakazi wote nchini kwa kuadhimisha sikukuu hii, na nawashukuru tena kwa mchango wenu adhimu katika ujenzi wa Taifa letu. Kama yalivyo makundi mengine kwenye jamii, kundi la wafanyakazi lina mchango mkubwa sana katika ujenzi wa nchi yetu. Serikali itaendelea kuimarisha mazingira ya kazi ikiwemo kuboresha maslahi ya wafanyakazi kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu.

Wito wangu kwenu wafanyakazi, ni kuendelea kutekeleza majukumu yenu kwa bidii, maarifa, uadilifu na kwa moyo wote, huku mkitanguliza maslahi ya Taifa mbele. Nawaomba pia muendelee kuongeza tija katika utendaji kazi. Navisihi vyama vya wafanyakazi tushirikiane na Serikali na Waajiri kuhakikisha tunaongeza tija kwenye maeneo yetu ya kazi kwa manufaa ya Taifa na wafanyakazi wenyewe, sambamba na kupaza sauti kuhusu madai ya wafanyakazi.

***Mungu Ibariki Afrika***
***Mungu Ibariki Tanzania***
***Kazi Iendelee.***